

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA
MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA



**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO
INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE,
VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1))

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaa ya Bunda
anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha
vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu,

ambapo jumla ya Shilingi **262,818,143.06/=** zimetengwa katika robo ya Kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025 Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi za serikali za mitaa zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- (i) Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na halmashauri,
- (ii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali,
- (iii) Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya menejimenti ya halmashauri

itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,

- (iv) Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na
- (v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.


Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (**tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na afisa maendeleo ya jamii wa kata husika au mtendaji wa kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo; barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na afisa mtendaji wa kijiji/mtaa, muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, andiko rahisi la mradi

unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo na taarifa ya akaunti ya benki.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 27 mwezi 10 mwaka 2024

Tangazo hili limetolewa na: -



George S. Mbilinyi

**MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA
BUNDA**